UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TANZANIA EDUCATION AUTHORITY

(Mamlaka ya Elimu Tanzania) (TEA)

BILIONI 2.2 KUTUMIKA AWAMU YA PILI YA MAFUNZO YA KUONGEZA UJUZI KWA VIJANA WANAOTOKA MAKUNDI MAALUM NA KAYA MASKININI (BURSERY SCHEME) NCHINI.

Zanzibar **12 Desemba 2022**

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Lela Mohamed Mussa leo tarehe 14 Desemba 2022 amezindua Mpango wa Ufadhili wa Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi kwa Vijana kutoka Makundi Maalumu na Wanaoishi Katika Mazingira Magumu (***Bursary Scheme for Vulnerable Groups***) katika hafla iliyofanyika katika viwanja vya Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknojia (KIST) Zanzibar.

Mpango huu wa Ufadhili unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) chini ya Mradi wa Elimu na Ujuzi kwa ajili ya Ajira zenye Tija (Education and Skills for Productive Jobs-ESPJ) unaoratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. SDF inafadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia.

TEA imepewa jukumu la kusimamia na kutekeleza Mpango huu na Wizara mama ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuwafikia vijana kutoka makundi maalumu na wanaoishi katika mazingira magumu walio katika kaya zilizosajiliwa na TASAF kuhakikisha wanafaidika na mpango huu kwa kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kujikwamua ki-uchumi.

Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Ufadhili *Bursary Scheme* ilitekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo ruzuku kiasi cha **Sh. Bl. 1.1** kimetolewa kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya kuendeleza ujuzi na stadi za kazi kwa wanufaika **1,627** (wanawake **518** na wanaume 1,109) ikijumuisha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu wanaoishi katika mazingira magumu.

Awamu ya pili ya Mpango Ufadhili wa Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi kwa Vijana kutoka Kaya Maskini na Wanaoishi katika Mazingira Magumu inaendelea katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 ikilenga kufadhili vijana **2,373** kutoka Tanzania Bara na Tanzania visiwani.

Miongoni mwao vijana **1,299 watatoka** Tanzania bara wakati **600** sawa na asilimia 25% watatoka Tanzania Zanzibar (300 kutoka Unguja na 300 kutoka Pemba0. Mpango huo pia utawanufaisha watu wenye ulemavu ni **474**. Jumla ya **Sh. Bl 2.2** zimepangwa kwa ajili ya utekelezaji wake.

Vigezo vilivyotumika kupata wanufaika ni pamoja na; muhusika kuwa na amesajiliwa katika kanzi-data (Database) ya TASAF, umri kati ya miaka 15 na 35 (au kufikia umri wa miaka 40 kwa watu wenye Ulemavu) na asiwe amedahiliwa na anahudhuria mafunzo mengine

Vigezo vingine vilivyotumika ni pamoja na mnufaika kuwa na na uwezo na msukumo wa kumaliza mafunzo, kukidhi vigezo vinavyohitajika kudahiliwa katika kozi husika na kuwa tayari kutoa taarifa kwa SDF zinazohusu mafunzo anayohudhuria na kuwa raia wa Tanzania.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya Umma inayofanya kazi chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. TEA inaratibu Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao unasaidia jitihada za Serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu kwa lengo la kuongeza ubora wa

elimu na upatikanaji wake kwa usawa. Pia TEA inaratibu Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia.

IMETOLEWA NA
KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO
Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)